THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

NOVEMBER 1997

021

# KISWAHILI

(For both School and Private Candidates)

MUDA: Saa 3

---

## MAAGIZO

1. Jibu maswali MANANE (8) tu, maswali MANNE (4) kutoka Sehemu A, na maswali YOTE ya Sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A: FASIHI

### Kifungu (i) Fasihi Simulizi.

1. "Fasihi Simulizi ina tanzu za Watoto na Watu Wazima". Chagua tanzu mbili za watoto na tanzu tatu za watu wazima kisha eleza faida na hasara kwa jamii inayohusika.

2. Maendeleo ya Sayansi na teknolojia yanaathirije Fasihi Simulizi ya Watanzania?

## FASIHI ANDISHI

### Kifungu (ii) Ushairi.

| | |
|---|---|
| Mashairi ya Chekacheka | - T.A. Mvungi (ESCO) |
| Mashairi ya Saadani | - S.A. Kandoro (MP LTD) |
| Teuzi za Nafsi | - F.H.J. Semghanga (TUKI). |

3. Jadili uwanadini wa waandishi wa ushairi wawili kati ya waandishi waliotajwa hapo juu.

4. Jadili matumizi ya tamathali za semi tatu katika vitabu viwili vya ushairi kati ya vitabu vilivyotajwa hapo juu.

### Kifungu (iii) Riwaya/Hadithi

| | |
|---|---|
| Kuli | - S.A. Shafi (T.P.H.) |
| Shida | - N. Balisidya (DUP) |
| Kusadikika | - S. Robert (NELSON) |

5. Kwa kutumia vitabu viwili vya hapo juu onesha jina na kitabu linavyohusiana na kinachozungumziwa.

6. "Ama kweli, bahati ya mwenzio usiilaliye mlango wazi". Usemi huu unahusu vitabu gani viwili? Fafanua kwa undani kwa kutumia vitabu hivyo hapo juu.

### Kifungu (iv) Tamthiliya

| | |
|---|---|
| Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe | - E. Semzaba (ESC) |
| Harakati za Ukombozi | - P. Muhando (TPH) |
| Hawala ya Fedha | - A. Lihamba (TPH). |

7. "Kukosekana kwa uadilifu katika uajibikaji ni kero kubwa kwa jamii". Thibitisha kauli hii kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya hizo hapo juu.

AU

8. Chagua wahusika wawili kutoka tamthiliya mbili za hapo juu, mhusika mmoja kutoka kila tamthiliya ili uoneshe jinsi gani wahusika hao wanavyostahili kulaumiwa na jamii.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU B: LUGHA

9. UFAHAMU:

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali.

Siti alikuwa na tabia ya kuajabiwa ingawa alikuwa mwanamke. Kama wanawake wengine walikuwa na umasikini wa johari hii, yeye alikuwa na ukwasi wake. Alikuwa katika nuru ya tabia wakati baadhi ya wanaume na wanawake walipokuwa katika giza lake. Katika milki kama hii alionekana na amani na upole, saburi na unyenyekevu, uungwana na uaminifu kwa watu wa kila rika na wa hadhi mbalimbali. Alikuwa kipenzi kikubwa. Katika maisha yake mwanamke huyu alikuwa katika mwendo wa tabia. Kama tabia yake ilihesabiwa kama gari, angalisemwa kwamba gari lenyewe lilitengenezwa vizuri sana. Lilikuwa na kiunzi cha saburi, mtambo wa bidii, magurudumu ya nguvu, sukani ya adili na siwa ya ucheshi. Katika gari hili Siti alivuta hawa na maendeleo ya watu toka kila upande kwa kipawa chake kikubwa cha sauti.

Kama Siti hakuwa na tabia ya namna hiyo, tegemeo lake lingalikuwa dogo sana katika maisha aliyoishi. Haijulikani angaliwezaje kujiokoa katika hatia isiyosameheka alipokuwa katika hasira na uchungu wa matusi! Hapana shaka kwa matukano yale yaliyorarua kama kucha za chuma katika moyo wake, alikuwa katika maudhi yasiyoelezeka kwa lugha ya kitabu; lakini alivumilia. Alijua kwamba ilimpasa kupigana na wivu, masingizio, kashfa, ujinga na ulimwengu mzima kama alitaka kufanikiwa. Alikuwa mwanamke mmoja katika wanawake waliokuwa imara kabisa.

Siti alikuwa mwanamke wa tabia kubwa ambayo hakuna kitabu cha Kiswahili kilichofundisha habari zake: kama aliipata kwao nyumbani au katika unyago inatatiza kuhakikisha kwa sababu wasimulizi wake wote wamenyamaza kimya juu ya jambo hili. Siti hakujua wajibu akauacha kuutimiza. Hakutumia tabia kama kisingizio au josho baada ya kujichafua kwa tamaa za aibu. alikuwa na imani nayo siku zote. Hakusema uwongo, hakujilegeza, hakujipendekeza wala kujifanya mtumwa. Alifanya kazi kila siku akajipatia usitawi kwa matendo yake mwenyewe. Bila shaka alichukua miaka mingi kufikia usitawi wake, lakini hakushindwa. Na kila siku aliweza kulaza kwa amani kichwa chake juu ya mto, bila kusumbuliwa na mawazo mabaya. Lipi lililokuwa bora kwa mwanamume au mwanamke kuliko kutazama nyuma ya maisha yake akayaona safi kama yungiyungi? Siti na tabia yake walikuwa kama marafiki wawili ambao waliafikiana kabisa katika maisha.

MASWALI:

(a) Toa maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

(b) Taja sifa kuu 3 za Siti.

(c) Nini kiliwavutia watu zaidi kwa Siti?

(d) Mwandishi ana maana gani anaposema,"Haijulikani angewezaje kujiokoa katika hatia isiyosameheka".

(e) Siti aliwezaje kujisitawisha?

(f) Toa kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu.

(g) Andika muhtasari wa maneno yasiyozidi 45 juu ya aya ya mwisho ya habari hii uliyoisoma.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

10. Andika insha isiyopungua maneno 250 juu ya mada moja zifuatazo:

(a) Udhalilishaji wa watoto.

(b) Kuhifadhi maji ni kuhifadhi uhai.

(c) Umuhimu wa Kiswahili nchini Tanzania.

(d) Rushwa ni adui wa maendeleo.

11. Bainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

(a) Juma ni mvivu sana.

(b) Ng'ombe huyu ana matata sana.

(c) Ah Nimeumia.

(d) Kucheza kunafurahisha watazamaji.

(e) Anakusubiri chumbani.

12. Sentensi zifuatazo zina makosa kwa kuzingatia usanifu wa Kiswahili. Pigia mstari hilo neno lenye kosa na juu yake andika neno sahihi katika kitabu chako cha kujibia.

(a) Mtoto angepelekwa hospitali angelipona.

(b) Mzee Nassoro ana ukwasi mno hivyo uwezo wa kununua gari hanao.

(c) Kifaranga kinapekuwa bila kufundishwa.

(d) Msichana mwenye nzuri tabia ni wa kuoa.

(e) Wanafunzi wa mashule yote ya Tanzania watakutana Dar es Salaam.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner